TANGAZO LA SERIKALI NA. 94 la tarehe 9/2/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16 (1))*

## MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA VIBALI VYA BURUDANI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA YA MWAKA, 2024

Jina

TS Na. 892 la 2023

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Vibali vya Burudani ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga ya Mwaka 2024, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ada na Vibali vya Burudani ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga ya Mwaka 2023 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho ya Jedwali la kwanza

2. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kufuta na kuandika upya Jedwali la Kwanza kama ifuatavyo:

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(2))*

ADA YA KUENDESHA SHUGHULI ZA BURUDANI

| Namba | Aina ya Shughuli | Kiwango cha Ada kwa Shilingi |
|---|---|---|
| 1. | Muziki wa Dansi, disko, taarabu na aina nyingineyo yoyote | Sh. 50,000/= kwa siku |
| 2. | Shindano la kutafuta msanii | Sh. 30,000/= kwa shindano |
| 3. | Shindano la kutafuta warembo | Sh. 50,000/= kwa shindano |

*Tangazo La Serikali Na. 94 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 4. | Maonesho ya mavazi | Sh. 50,000/= kwa onesho |
| 5. | Maombi ya kibali cha sherehe za unyago, ngoma na harusi na sherehe nyingine yoyote | Sh. 30,000/=kwa sherehe |
| 6. | Matangazo ya kuuza bidhaa zinazopungua bei (promotion) | Sh. 50,000/= kwa tangazo |
| 7. | Matamasha ya kibiashara | Sh. 1,500,000/= kwa tamasha |
| 8. | Matangazo madogo | Sh. 30,000/= kwa tangazo |
| 9. | Maonesho ya sinema na video | Sh. 500/= kwa siku |
| 10. | Matamasha yasiyo ya kibiashara | Sh. 100,000/= kwa tamasha |
| 11. | Kupiga picha za video | Sh. 10,000/= kwa kila tukio |
| 12. | Mchezo wa fete/Bahatinasibu | Sh. 30,000/= kwa Mwezi |

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatiaazimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga uliofanyika Tarehe 29 Mwezi 11 Mwaka 2022 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:

RASHID GEMBE
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga*

AMANI J. KASINYA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga*

NAKUBALI,

Dodoma,
2 Februari, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)
*Waziri Wa Nchi - Ofisi Raisi,*
*(Tawala Za Mikoa Na Serikali Za Mitaa)*